**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHESHIMIWA MAGALULA SAID MAGALULA ALIPOZINDUA BODI YA NNE YA MAJI BONDE LA ZIWA RUKWA KATIKA UKUMBI WA LIBORI MJINI SUMBAWANGA TAREHE 17 DESEMBA, 2015**

***Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Engineer Ngosi Mwihava,***

***Mwenyekiti wa Bodi ya Nne ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, Bw Lawrence Mbuya,***

***Wajumbe wa Bodi ya Nne ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa,***

***Menejimenti ya Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa,***

***Wageni waalikwa,***

***Wanahabari,***

***Mabibi na Mabwana.***

## 1.0 Utangulizi

**Wajumbe wa Bodi,** awali ya yote kwa namna ya pekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kwa kukutana siku ya leo tukiwa salama. Kwa wale waliotoka nje ya Mkoa wetu wa Rukwa poleni sana na uchovu wa safari karibuni sana katika Mji wetu wa Sumbawanga.

**Wajumbe wa Bodi,** napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wajumbe kwa uteuzi wenu. Hongereni sana kwa sababu Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Maji amewaona mnafaa kukabidhiwa majukumu haya mazito ya

kuongoza shughuli za Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde letu la Ziwa Rukwa.
Aidha, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Bodi na Wizara kwa kunipa heshma hii ya kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi wa Bodi hii ya Nne ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa. Niwashukuru pia kwa uamuzi wenu wa kufanyia uzinduzi na kikao chenu cha kwanza hapa Sumbawanga katika Mkoa wa Rukwa.

## 2.0 Sura ya Bonde la Ziwa Rukwa.

**Wajumbe wa Bodi,** Bonde la Ziwa Rukwa ni Bonde ambalo linaingiza Maji kutokea kwenye vijito vidogo vidogo kuingia kwenye Ziwa Rukwa. Ziwa lina eneo la Kilometa za Mraba zipatazo 2,300 na Bonde zima lina ukubwa wa Kilometa za Mraba 88,000.

Bonde la Ziwa Rukwa limegawanyika katika Wilaya za Sumbawanga, Nkasi, Chunya, Momba, Mlele, Mpanda na Sikonge. Natambua tabia za Bonde ni za mfumo wa Bonde la Ufa la Afrika Mashariki. Upande wa Magharibi wa Ziwa upo katika miinuko ya Ufipa. Upande wa Kaskazini wa Bonde umeinuka kuelekea upande wa Bonde wa Ziwa Tanganyika, na upande wa Mashariki umetawaliwa na safu ya milima ya Mbeya.

Bonde hili lina wakazi wapatao zaidi ya Millioni mbili nukta tano ambao wapo katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Katavi na sehemu ndogo za Mikoa ya Tabora na Singida.

**Wajumbe wa Bodi,** ni dhahiri kwamba Bonde la Ziwa Rukwa lina umuhimu katika ustawi wa maisha ya Wananchi wa Mikoa na maeneo kama nilivyoyaanisha hapo juu.

## 3.0 Majukumu ya Bodi

**Wajumbe wa Bodi,** kwa mujibu wa sheria inayoiunda Bodi hii, kazi za Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa (kama zilivyoorodheshwa kwenye kifungu cha 23 cha Sheria) ni pamoja na;

***Kwanza,*** kuandaa mipango ya pamoja ya usimamizi na uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde (Integrated Water Resources Management and Development Plans) inayojumuisha na mipango ya Wilaya zote zilizoko kwenye Bonde.

***Pili,*** kuandaa miongozo na viwango vya ujenzi wa miundombinu ya kuchukulia maji toka kwenye vyanzo katika Bonde na kusimamia utekelezaji wake.

***Tatu,*** usimamizi wa data na taarifa za Usimamizi wa Rasilimali za Maji na kufanya tathmini ya mara kwa mara kuhusu upatikanaji wa maji na mahitaji yake.

***Nne,*** kugawa maji (kupitia vibali) na kufuatilia utekelezaji wake, pia kuzuia uchafuzi wa vyanzo vya maji.

***Tano,*** kutatua migogoro ya maji ndani ya Bonde.

***Sita,*** kuratibu usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa sekta zingine katika Bonde.

***Saba,*** kumshauri Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kuhusu masuala ya Maji Shirikishi kwenye Bonde.

## 4.0 Hali ilivyo sasa katika Bonde la Ziwa Rukwa

**Wajumbe wa Bodi,** kama mlivyosikia majukumu ya Bodi yenu, ni wazi mbele yenu kuna kazi kubwa ya kufanya ili muweze kusimamia Rasilimali za maji katika Bonde hili kikamilifu.
Hata hivyo, Bonde letu lina maeneo kadhaa yanayohitaji kurekebishwa maeneo hayo ni pamoja na;

i. Uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana na shughuli za kibinadamu hasa kuendesha kilimo cha bustani za mbogamboga na mahindi (hapa Sumbawanga kuna mto Lwiche na vyanzo vyake unaendelea kuharibiwa na shughuli za kibinadamu, mto Lupahuko Chunya umeathiriwa vibaya sana.

ii. Matumizi holela ya maji bila vibali (hasa mto Katuma-Mpanda.)

iii. Ongezeko kubwa la watu hasa vijiji vya pembeni ya Bonde la Ziwa Rukwa.

iv. Tija ndogo katika matumizi ya maji hasa miradi ya umwagiliaji.

v. Miundombinu ya uchunguzi wa Rasilimali za Maji bado ni duni.

vi. Uharibifu wa mazingira pembeni ya Bonde la Ziwa Rukwa unaosababishwa na wingi wa mifugo na shughuli za kilimo.

vii. Taasisi za ngazi ya chini za usimamizi wa Rasilimali za Maji (Jumuiya za Watumia Maji, Kamati za Maji za Mabonde Madogo) bado hazijaanzishwa za kutosha.

## 5.0 Ziwa kama kitovu cha Bonde hili.

**Wajumbe wa Bodi,** Ziwa Rukwa linapatikana kwenye maeneo ya Mkoa wa Mbeya, Rukwa na Katavi. Kwa Mkoani Mbeya Ziwa lipo Kaskazini mwa Wilaya ya Momba na Wilayani Chunya lipo Magharibi mwa Wilaya hiyo.

Kilometa za mraba 292 sawa na asilimia 28.9 ya Ziwa hilo zinapatikana Wilayani Momba. Kilometa za mraba 718 sawa na asilimia 71.1 zipo upande wa Wilaya jirani za Chunya, Sumbawanga na sehemu ya Mkoa wa Katavi.

Kama ilivyo kwa maziwa mengine Nchini, Ziwa Rukwa lina mchango mkubwa katika maendeleo ya Jamii ziishizo jirani nalo na Taifa kwa ujumla.

**Wajumbe wa Bodi,** Ziwa hilo linachangia katika pato la mtu mmoja mmoja na Taifa kupitia shughuli za Uvuvi, Usafiri wa majini na pia upatikanaji wa kitoweo aina ya samaki. Bonde la Ziwa hilo pia limekuwa kichocheo kikubwa katika shughuli za kilimo na ufugaji. Mazao aina ya Mpunga, Mahindi, Ufuta, Ulezi,

Mtama nk. hustawi vizuri kwenye Bonde la Ziwa hilo kutokana na udongo wenye rutuba na maji ya mito mikubwa ikiwemo ya Mfwizi, Lwiche, Momba na Rupa ambayo hutumika katika shughuli za kilimo.

**Wajumbe wa Bodi,** hata hivyo, Ziwa Rukwa limewekwa kwenye orodha ya Rasilimali ambazo ziko katika hatari ya kupotea endapo hazitafanyika juhudi kuliokoa. Taarifa kutoka vyanzo mbalimbali zinabainisha kuwepo kwa viashiria vya kukauka kwa Ziwa, ikiwa ni pamoja na kupungua kwa ubora wa maji katika Ziwa hilo na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu.

Utafiti wa mwisho unaoonesha kwamba kina cha maji cha Ziwa Rukwa kimepungua kutoka mita ishirini mwanzoni mwa miaka ya themanini hadi mita tisa sasa.

**Wajumbe wa Bodi,** tahadhari za makusudi zisipochukuliwa Ziwa Rukwa linaweza kupotea kabisa. **Naiomba Bodi hii inayozinduliwa leo kuainisha mikakati ya kuliokoa Ziwa Rukwa ili malengo ya kuanzisha Bonde la Ziwa Rukwa yaweze kutimia.**

## 6.0 Jukumu lililo mbele yenu

**Wajumbe wa Bodi**, ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo zote, ni lazima usimamizi wa Rasilimali za Maji ufanywe kwa pamoja kwa kupitia dhana hii ya Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji (UPARAMA).

Dhana hii inajumuisha mchakato wa Maendeleo Endelevu (Sustainable Development), Ugawaji Maji (Water Allocation) na Ufuatiliaji wa Rasilimali za Maji (Water Resources Monitoring)

kwa malengo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira ili kuleta matokeo chanya.

## 7.0 Wito kwa Watumishi wa Menejimenti ya Bonde la Ziwa Rukwa.

- Tekelezeni majukumu yenu kwa kuzingatia viwango mlivyojiwekea na vigezo vya utendaji vilivyowekwa na sekta ya maji.
- Fanyeni kazi kwa ustadi, kwa kutumia weledi, kwa kuzingatia nidhamu na taaluma zenu.
- Vile vile tumieni muda wenu, kujiendeleza kitaaluma ili kufikia viwango vya utendaji na malengo kwa mujibu wa Mpango Kazi.

## 8.0 Hitimisho.

**Wajumbe wa Bodi,** ili kuweza kutekeleza hayo yote, Ushirikiano katika ngazi zote ni muhimu sana ili kuweza kufanikisha majukumu ya Bodi hii. Ninacho ahidi kwenu ni utayari wa Ofisi yangu kutoa msaada unaotakiwa katika kuhakikisha kwamba usimamizi wa sheria zote hauchezewi na yeyote.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa itaendelea kutoa ushirikiano kwa wadau mbalimbali Mkoani katika shughuli za maendeleo (Kiuchumi na Kijamii).

**Wajumbe wa Bodi,** muda wote Ofisi iko wazi kwa kila Mdau kuwasilisha mapendekezo na mawazo yake katika kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa ufanisi zaidi.

**Wajumbe wa Bodi,** wakati nahitimisha sasa, nawatakieni kila la kheri katika kutekeleza majukumu yenu kama wajumbe wa Bodi ya Bonde la Ziwa Rukwa.

**Wajumbe wa Bodi,** baada ya kusema maneno hayo, sasa nachukua fursa hii kutamka kwamba **Bodi ya Nne ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa** imezinduliwa Rasmi.

**Maji ni Uhai,**

**Utunzaji wa mazingira ni ustaarabu.**

**Asanteni kwa kunisikiliza**